

Jina: .....

Nambari: .....

Sahihi .....

Tarehe: .....

102/3

**KARATASI YA TATU**

**FASIHI**

**MUDA: SAA 2<sup>1/2</sup>**

# **MTIHANI WA PAMOJA WA MWIGO WILAYA YA KHWISERO**

*Hati ya kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)*

**KISWAHILI**

**Fasihi**

**MAAGIZO:**

1. *Jibu maswali MANNE pekee*
2. *Swali la kwanza ni la LAZIMA*
3. *Chagua maswali mengine matatu kutoka sehemu zilizosalia*
4. *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*
5. *Kila swali lina alama 20*

*Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

**Swali la lazima-  
SEHEMU YA A-USHAIRI .**

Baba amenisomea, barua yenye thamani,  
Mama kaniandikia, kinda niliye mtini,  
Tabu haijanitoa, mama yangu simuoni,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.

Sauti uliyotoa, imenigusa moyoni,  
Mara kuikumbukia, haingia kilioni,  
Nalia mie Radhia, mama yangu simuoni,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.

Maneno kayasikia, hadhani uko mekoni,  
Mbio nikachungulia, nikalia sikuoni,  
Huzuni imeningia, mama nitafanya nini?  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.

Kuku anaangalia, vitoto vyake uani,  
Kimojapo kikilia, hatulii asilani,  
Yuko radhi kujifia, chanawe kukiauni,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.

Hata paka nakwambia, si mbwa wala si nyani  
Kamwe hawatakimbia, kuacha wana mtini,  
Lakini mie Radhia, nimetupwa majanini,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.

Hizi tunu za dunia, zisikufanye haini,  
Wengi wanazililia, na haweshi usikini,  
Asipokupa Jalia, hukupata asilani,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.

Wangapi wamepumua, wenye urembo wa shani,  
Ngoma walijichezea, wakakita furahani,  
Zao zimejishia, hako wa kuwathamini,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.

Haya yamekuchochea, uniache majanini,  
Mwanao mie Radhia, nibakie ukiwani,  
Mama utasimulia, kesho, mbele ya Manani,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.

Kinda ninashitakia, kwa Wadudi Rahamani,  
Sumbukuku naumia, sasa nimo msibani,  
Mama umenikimbia, nimekosa neon gain?  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.

Nimekonda kwa kulia, ghuma haishi moyoni,  
Pengine nitajifia, kwa majonzi na huzuni,  
Usije kunililia, nizikwapo kaburini,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia

### **Maswali**

- (a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (al.2)
- (b) Fafanua toni ya shairi hili (al.2)
- (c) Nini kinachosabababisha hali ya mtunzi (al.4)
- (d) Huku ukitoa mifano **miwili** tambua mbinu zilizotumika katika shairi hili (al.4)
- (e) Andika ubeti wa tisa kwa lugha ya nathari (al.4)
- (f) Eleza aina **moja** ya uhuru wa kishairi (al.2)
- (g) Eleza maana ya msamiati huu jinsi ulivyotumika katika shairi (al.2)
- (i) ghuma-
- (ii) Sumbukuku-

### **SEHEMU ZA B : RIWAYA**

#### **SAID A. MOHAMMED: UTENGANO**

#### **Jibu swali la 2 au 3**

2. “Ndivyo bwana lakini Mungu ataleta heri yake“
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)
- (b) Msemaji alileta ujumbe maalum ukitoa mifano **mitatu** elezea (al.8)
- (c) Eleza tabia ya msemaji (al.6)
- (d) Baada ya usemi huu msemewa aliitikia uamuzi fulani fafanua. (al.2)

### **Au**

3. Ukitoa mifano mwafaka , eleza matumizi ya mbinu zifuatazo katika riwaya ya *Utengano*
- (i) Sadfa (al.10)
- (ii) Kinaya (al.6)
- (iii) Methali (al.4)

### **SEHEMU YA C: TAMTHILIA**

#### **TIMOTHY M. AREGE MSTAHIKI MEYA**

#### **Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Watu wenye matumbo yasiyotulia huwa akili zao nazo hazitulii.....Jambo hili ni hatari kwa kiongozi yeyote .."
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)
  - (b) Eleza chanzo cha hatari inayozungumziwa (al.6)
  - (c) Msemaji anatoa tahadhari kwa msemewa. Ifafanue (al.4)
  - (d) Msemewa anachukua hatua ipi kukabiliana na ujumbe huu (al.4)
  - (e) Eleza mbinu inayojitokeza katika usemi huu (al.2)

Au

5. Tamthilia ya *Mstahiki Meya* inaangazia hali halisia inayokumba nchi nyingi. Huku ukitoa mifano kumi kitabuni thibitisha ukweli wa kauli hii. (al.20)

**SEHEMU YA D: Hadithi Fupi Damu Nyeusi**

6. a. Huku ukirejelea hadithi ya *Mke Wangu*. Eleza maoni ya wahusika wafuatao kuhusu maisha
- (i) Aziza (al.5)
  - (ii) Mwandishi (al.5)
  - (b) Mbinu ya kinaya na maswali ya balagha imetamalaki katika hadithi hii. Ukitoa mifano **Mitano** kwa kila mbinu thibitisha kauli hii

(al.10)

**7. SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

- (i) Eleza maana ya ngano (al.4)
- (ii) Tambua na ufafanue migao miwili ya kipera cha ngano (al.4)
- (iii) Taja na ueleze aina **tatu** za ngano (al.6)
- (iv) Eleza umuhimu wa ngano (al.6)

**ANSWERS:**

Order a copy of answers from [www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy](http://www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy)

NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs